# MAFUA YA NDEGE




## MAELEZO KWA UMMA JUU YA

## MAFUA YA NDEGE

INTERNATIONAL CENTRE FOR MIGRATION AND HEALTH

Partner for Global Health
TaiwanIHA
Taiwan International Health Action


## Kwa nini kijitabu juu ya mafua ya Ndege kinahitajika?

Wakati wowote dunia inapokabiliwa na vitisho vipya vya kiafya kunakuwa na wasiwasi kuwa uvumi usiokuwa wa kweli unaweza kusababisha milipuko ya hofu. Homa ya mafua ya ndege yanayotokana na kirusi cha H5N1 au kama yalivyozoeleka kuitwa mafua ya ndege, ni moja kati ya vitisho hivyo vya kiafya. Maelezo haya yanaweza kusaidia watu kuelewa mafua ya ndege ni nini  na nini cha kufanya juu yake.

## Homa ya mafua au mafua ni nini?

Homa ya mafua au "mafua" hutokana na kirusi ambacho hushambulia mfumo wa upumuaji. Ni ugonjwa wa kuambukiza na unaweza kuenea kwa haraka

## Homa ya mafua ya ndege au mafua ya ndege ni kitu gani?



Homa ya mafua ya ndege kwa kawaida huitwa 'mafua ya ndege.  Mafua ya ndege ni ugonjwa ambao kwa kiwango kikubwa huambukizwa miongoni mwa ndege, kwa kawaida huenezwa kutoka ndege mmoja hadi mwingine. Mafua ya ndege yanafikiriwa kuwaathiri ndege wote, wa mwituni na wa nyumbani.  Katika hali ambapo ugonjwa haujafikia hatua mbaya, mafua ya ndege yanaweza kutokea miongoni mwa ndege wanaohamahama bila kuwa na dalili ya wazi na kunakuwa na madhara madogo yakiwemo yanayoathiri mfumo wa upumuaji. Mafua ya ndege yakiwa makali yanaweza kuathiri mfumo wa upumuaji wa ndege, yanashambulia viungo vingi na yanaweza kusababisha kifo cha ndege.

Hivi karibuni,  aina mpya ya kirusi kinachosababisha mafua ya ndege kinachoitwa "H5N1" kimejitokeza. Kirusi

hicho kinasababisha ugonjwa mbaya na umeenea miongoni mwa ndege duniani kote. Mafua ya ndege ya H5N1 yamefanya baadhi ya ndege wanaohamahama na wale wanaofugwa majumbani kama kuku na mabata kuugua sana na hatimaye kufa.

## Maambukizo ya mafua ya ndege ya H5N1 kwa binadamu

Hivi sasa kirusi cha H5N1 ni jambo zito linalohangaisha kuhusiana na afya ya binadamu. Kirusi cha H5N1 ni ugonjwa mkali, na katika hali isiyo ya kawaida, umevuka mipaka kwa kuenea kutoka kwa ndege kwenda kwa binadamu. Hivi sasa, zaidi ya watu 100 wameambukizwa kirusi cha mafua ya ndege cha H5N1 na wamefariki kutokana na ugonjwa huo. Kirusi cha H5N1 kwa sasa hakiambukizwi kwa urahisi kutoka kwa ndege kwenda kwa binadamu. Hata hivyo, hali inaweza ikabadilika, na watu wengi zaidi wanaweza kuambukizwa kwa haraka sana.

***Kirusi cha H5N1 pia kinapatikana kwa kugusana na ndege mgonjwa au aliyekufa mwenye mambukizo***

## Jinsi gani watu hupata mafua ya ndege kwa sasa?

Kinachojulikana kwa sasa ni kuwa binadamu anaambukizwa kirusi cha mafua ya ndege cha H5N1 wakati anapokuwa na mguso wa moja kwa moja na ndege walioambukizwa ugonjwa huo, au ndege waliokufa, au kugusa sehemu na vitu vilivyochafuliwa na vinyesi vya ndege. Mafua ya ndege yanaweza pia kuambukizwa kutokana na maji maji ya puani na mate ya ndege waliokufa au ndege walio hai wenye maambukizo na kutoka katika sehemu zilizochafuliwa na uchafu wa maji maji au maji maji toka katika mwili wa ndege.

Kwa mfano, kumekuwepo matukio machache ambapo inafikiriwa kwamba watoto waliambukizwa kirusi cha mafua ya

ndege cha H5N1 kutoka katika vinyesi vya kuku, mabata, n.k kwa vile walicheza maeneo ambayo kulikuwa na ndege hao.

## Mafua ya ndege yanawaathirije watu?

*Pika kuku na mayai kikamilifu*

Katika matukio machache ambapo hivi karibuni watu waligusana na ndege wenye maambukizo, walipata mafua ya ndege ya H5N1. Watu hao walikuwa na dalili kama vile homa (kiwango cha chini kilikuwa ni nyuzi joto 38 za selisiasi), kikohozi, kukosa pumzi ya kutosha, kupumua kwa shida na wakati mwingine walipata nimonia. Pia kumekuwepo na taarifa juu ya dalili nyingine kama vile kuharisha, kutapika, maumivu ya tumbo, maumivu ya kifua, viungo vingi kushindwa kufanya kazi vizuri, na kutokwa na damu puani na kwenye fizi. Matukio mengi yaliyotolewa taarifa yametokea kwa watoto na vijana ambao awali walikuwa wenye afya nzuri. Hadi sasa, kati ya watu wachache ambao wamepata mafua ya ndege ya H5N1, zaidi ya nusu wamefariki.

## Je, ni salama kula ndege kuku, mabata, n.k?

Binadamu hawatakuwa katika hatari ya kupata maambukizo ya H5N1 kwa njia ya chakula iwapo kuku, mabata, n.k na mayai yao vitashughulikiwa kwa njia ya usalama na kupikwa vizuri. Hata hivyo ndege ambao wanajulikana kuwa walikuwa wagonjwa, hawafai kuliwa hata kama watapikwa vizuri.

Wakati wote dumisha usafi unapoaandaa chakula kwa ajili ya kupika. Hakikisha kuwa chakula kilichopikwa kinahifadhiwa mbali na kuku, mabata, n.k ambao hawajapikwa au mayai yao, au weka mbali na vitu kama vyombo vya nyumbani vilivyochafuliwa na hao ndege. Osha mikono kabla na baada ya kuandaa chakula.

## Kuenea kwa mafua kwa binadamu duniani kote

Kuna uwezekano kwamba kirusi cha H5N1 kinaweza kukua na kuwa kirusi ambacho kinaweza kupita kwa urahisi toka kwa mtu mmoja kwenda kwa mtu mwingine na kuendelea kuenea kwa watu wengine. Hali hii ikitokea, mafua yanaweza kuenea kwenye nchi nyingi na kwa watu wengi na kwa kiwango kikubwa.



## Kitu unachoweza kufanya sasa

Magonjwa ya mfumo wa upumuaji kama vile mafua huenea kwa njia ya kikohozi or chafya na mikono michafu. Ili kuzuia ueneaji wa mafua:

- Osha mikono yako kwa maji na sabuni
- Funika mdomo wako na pua yako wakati unapokohoa au unapopiga chafya
- Punguza matembezi yako endapo kuna mlipuko wa mafua ya ndege katika eneo lako.

## Osha mikono yako kwa maji na sabuni


Uoshaji wa mikono huzuia kuenea kwa maambukizo. Osha mikono yako kwa maji na sabuni hasa:

- Baada ya kukohoa au kupiga chafya.
- Kabla na baada ya kutayarisha chakula. Pia safisha sehemu za kuandalia chakula na vyombo vya nyumbani kwa kutumia maji na sabuni
- Kabla na baada ya kuwalisha watoto,
- Baada ya kutoka chooni, na
- Baada ya kuwaogesha au kuwasafisha watoto

Endapo hakuna sabuni, tumia majivu badala yake.

## Funika mdomo wako na pua yako wakati unapokohoa au unapopiga chafya

Kufunika mdomo na pua wakati unapokohoa au unapopiga chafya huzuia kuenea kwa maambukizo.



- Wakati wote funika pua yako na mdomo wako kwa kutumia nguo, skafu au taulo, au kwa kutumia mkono wa vazi kama vile koti au shati wakati unapokohoa au kupiga chafya. Tupilia mbali nguo, skafu, au taulo au zisafishe kwa maji na sabuni. Usikohoe au kupiga chafya kwenye mikono yako kwa sababu hii itaeneza mafua wakati unapogusana na vitu vingine au watu wengine.
- Epuka kukohoa au kupiga chafya wakati watu wengine wapo karibu nawe. Kaa mbali na watu wengine hadi utakapokuwa hauna dalili za matatizo katika mfumo wa upumuaji.
- Waombe watu wanaokohoa au kupiga chafya kufunika pua zao na midomo yao.

## Punguza matembezi yako

Kupunguza matembezi ya watu huzuia kuenea kwa maambukizo yeyote. Endapo kuna mlipuko au ikiwa hali ya mafua itakuwa mbaya katika eneo lako:

- Jilinde mwenyewe na wengine kwa kuepuka mikutano ya hadhara au sehemu za umma.
- Kaa mbali na watu wengine ikiwa wewe ni mgonjwa.
- Epuka kugusana na maji maji kutoka kwa watu ambao wana dalili za matatizo ya

mfumo wa upumuaji.

- Ishi mahali ambapo kuna uwezekano wa wewe kupata matibabu pale itakapohitajika.
- Endapo unamhudumia mtu mgonjwa, jilinde mwenyewe. Funika pua yako na mdomo wako na osha mikono yako kwa maji na sabuni kila baada ya kumhudumia mgonjwa. Pia epuka mgusano wa karibu na watu wengine katika kipindi ambacho mgonjwa yupo katika hatua mbaya ya kuweza kuambukiza wengine. (kama itakavyoshauriwa na mhudumu wa afya).

## Hatua nyingine za kuchukua

*Usiguse ndege waliokufa*

Kaa mbali na kamwe usiguse ndege waliokufa ambao unaweza kukutana nao. Toa taarifa juu ya ndege waliokufa kwenye mamlaka ya serikali ya mahali unapoishi.

Weka maeneo unayoishi katika hali ya usafi. Tumia dawa ya kuwa vijidudu kusafisha sehemu au vitu ambavyo vinaweza vikawa vimegusana na maji maji na uchafu wa maji maji kutoka katika mwili wa ndege aliye hai au aliyekufa mwenye maambukizo.

Kaa mbali kiasi kutoka walipo kuku, mabata, n.k. au ndege pori pamoja na vinyesi vyao. Epuka kuleta kuku, mabata, n.k walio hai karibu na eneo unaloishi.

Hifadhi kuku, mabata, n.k katika kizizi kilichofunikwa kwa paa ili kuzuia wasikutane na ndege au watu. Wazuie watoto wasicheze mahali ambapo kuku, mabata, n.k hufika mara kwa mara.

*Kaa mbali na masoko ya kuku*

Kaa mbali na maeneo ya kufugia kuku, mabata, n.k. pamoja na masoko ya kuuzia kuku ambako ndege huchinjwa na kusafishwa.

## Maelezo ya ziada

**Taarifa za karibuni kuhusu mafua ya ndege na maandalizi ya kukabiliana na ueneaji wake miongoni mwa binadamu duniani zinaweza kupatikana kupitia katika anwani zifuatazo:**

- http://www.who.int/csr/disease/avian_influenza/en/
- http://www.cdc.gov/flu/avian/gen-info/facts.htm
- http://www.reliefweb.int/rw/hlp.nsf/db900ByKey/avian_influenza?OpenDocument

**Maelezo haya yameandaliwa na ICMH kwa msaada kutoka TaiwanIHA.**

***13 Aprili 2006***

INTERNATIONAL CENTRE FOR MIGRATION AND HEALTH

Partner for Global Health
TaiwanIHA
Taiwan International Health Action

**Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na:**
**The International Centre for Migration and Health**
**11 Route du Nant d'Avril**
**CH-1214 Vernier (Ge)**
**Switzerland**
**Tel: + 41 22 783 1080 Fax: + 41 22 783 1087**
**Email: admin@icmh.ch**